



Org.no.802464-1378

Kumb. Na:TR20230317/01

## TANGAZO KWA UMMA

### SHEREHE YA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI JULAI 7, 2023 COPENHAGEN DENMARK

Baraza la diaspora Watanzania Sweden-Tanriks kwa kushirikiana na ubalozi wa Tanzania Stockholm Sweden, linawakaribisha wanachama na wakazi wote wa Sweden wenye mapenzi na utamaduni wa Kitanzania mahususi lugha ya kiswahili, kuhudhuria sherehe ya siku ya kiswahili dunia.

Sherehe itafanyika tarehe 7 Julai 2023 Copenhagen Denmark. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuendeleza utamaduni wetu na heshima kubwa tuliyopewa na UNESCO, tunawaomba wanachama na umma kushiriki kwa wingi ili kufanikisha sherehe hiyo.

Barua rasmi ya mwaliko ya Ubalози, imeambatanishwa hapa chini kwa taarifa zaidi. Kiswahili ni tunu ya Watanzania na tukutane Denmark kusherekea. Asanteni.

**Tanriks inawaleta Watu wote Pamoja.**

*EPedersen*

Elizabeth M. Pedersen  
Mwenyekiti  
Tanriks  
2023-06-10

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu Na: +46 8 732 2430/31  
Fax: + 46 8 732 2432  
Email: [mailbox@tanemb.se](mailto:mailbox@tanemb.se)  
Web: [www.se.tzembassy.go.tz](http://www.se.tzembassy.go.tz)

**Ubalozi wa Tanzania**  
Näsby Allé 6  
183 55 Täby  
Sweden

**Kumb Na: NA.38/605/01**

**14 Juni, 2023**

Kwa Viongozi wa Jumuiya zote za Watanzania,  
Eneo la Uwakilishi.


## **SHEREHE YA SIKU YA LUGHA YA KISWAHILI DUNIANI** **JULAI 7, 2023 COPENHAGEN, DENMARK**

Tafadhali husika na kishwa cha habari hapo juu.

Kama mnavyofahamu, Kikao cha 41 cha UNESCO kiliamua kutambua Lugha ya Kiswahili na kuifanya tarehe 7 Julai iwe siku ya kusherehekea matumizi ya lugha hii. Ubalozi utakuwa unandaa kila mwaka sherehe hizo, kwa mzunguko katika Nchi za Uwakilishi, kwa kushirikiana na Diaspora.

Kwa muktadha huo, Ubalozi unapenda kuwaarifu kwamba, Sherehe ya **SIKU YA LUGHA YA KISWAHILI DUNIANI** itafanyika tarehe 7 Julai, 2023 mjini Copenhagen nchini Denmark. Sherehe hii inaadaliwa na Ubalozi kwa kushirikiana na Tanzania Diaspora waishio nchini Denmark (TANDEN). Anuani na mahali sherehe itakapofanyika itatumwa kwenu na TANDEN hivi karibuni.

Hivyo, ninyi kama Viongozi wa Jumuiya za Watanzania waishio nchi za Uwakilishi, Ubalozi unawaomba muwafahamishe Wanachama wenu na kuwahamasisha kuhudhuria Sherehe hii nchini Denmark.

  
Dr. Edmund Kitokezi  
KNY: BALOZI

**TANRIKS INAWALETA WATU WOTE PAMOJA**